HOTUBA YA KUWASILISHA MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA NA USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

1. Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa kukutana leo hapa tukiwa wazima wa Afya. Aidha, kwa heshima kubwa nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuniruhusu kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma.

B Historia

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Mashirika ya Umma kwa lengo la

kuendesha biashara na kutoa huduma katika jamii ili kuimarisha uchumi na kurahisisha upatikanaji wa huduma. Katika kuyasimamia Mashirika hayo Serikali iliona haja ya kuanzisha sheria itakayosimamia Mashirika hayo. Hivyo, mnamo mwaka 1978 Serikali ilitunga sheria iitwayo “The Public Enterprises Decree” namba 4 ya mwaka 1978.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuekeza katika njia tofauti zikiwemo kununua hisa, kuingia mashirikiano ya kibiashara na Sekta binafsi pamoja na kuwekeza katika mitaji.Hali hiyo ilipelekea kuundwa kwa Sheria mpya ya mitaji ya Umma nambari 4 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo ya mwaka 2002 ilipelekea kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya

Umma pamoja na Kampuni za Serikali katika kuimarisha uchumi ambapo Mashirika hayo yaliweza kuengeza mapato ya Serikali kupitia ulipaji wa kodi mbalimbali, ulipaji wa gawio pamoja na kutoa ajira.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio yaliyopatika kupitia sheria hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeonekana ipo haja ya kupitiwa upya sheria hiyo kwa lengo la kuimarisha usimamizi zaidi wa Mali pamoja na Mashirika ya Umma.

3. Madhumuni

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya kuanzishwa kwa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na kufuta Sheria ya Mitaji ya Umma nambari 4 ya mwaka 2002 ni kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi, kutoa huduma bora

na hatimae kupelekea kuongezeka mapato ya Serikali kupitia gawio na kodi zitakazolipwa na mashirika hayo.

Aidha, Sheria hii inakusudia kuimarisha usimamizi wa mali za Umma kwa kuweka utaratibu wa kisheria unaoweka wazi majukumu ya kila ngazi katika usimamizi wa mali hizo.

4. Mantiki

Mheshimiwa Spika, Kutokana na Serikali kutambua mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Sheria iliyopo sasa ambayo yanajumuisha;-

1. Kuwepo kwa utaratibu wa kisheria usiojitosheleza wa kuzisimamia na kutathmini utendaji wa Taasisi zote zinazojitegemea zikiwemo Kampuni, Mashirika na Taasisi zenye kujiendesha kibiashara.

2. Kuwa na Ofisi ambayo haina mamlaka yenye kujitosheleza na kujitegemea kisheria katika usimamizi wa Taasisi na Mali za Umma,
3. Kukosekana kwa Taasisi yenye uwezo wa kutoa miongozo kwa Taasisi zinazojiendesha kibiashara kabla ya utekelezaji wa mipango yao.
4. Ufanisi mdogo wa utendaji wa baadhi ya mashirika hali inayopelekea kukosekana mapato ya Serikali,
5. Kuwepo uwajibikaji usiokidhi mahitaji kwa baadhi ya watendaji wakuu,wenyeviti na wajumbe wa Bodi wa Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia mapungufu hayo, Serikali imeona ipo haja ya kutunga Sheria mpya yenye lengo la:

1. Kuwa na Taasisi ambayo itatoa miongozo kwa Mashirika pamoja na Taasisi zilizoanzishwa na

Serikali kwa ajili ya kutoa huduma au kufanya biashara,

2. Kusimamia mipango ya kibiashara, bajeti, uwekezaji pamoja na mpango mkakati iliyopitishwa kwa ajili ya kuendesha Mashirika na Taasisi zinazotoa huduma za Serikali,
3. Kuwa na utaratibu wa kuingia mikataba baina ya Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi,
4. Kuwa na jukumu la kupitia na kuidhinisha mapendekezo ya miradi, Mashirika na Taasisi za Umma,
5. Kuwepo usimamizi imara wa mali za Umma kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya mali hizo.

5. Umuhimu wa Mswada

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa Sheria hii kutapelekea kupatika kwa faida zifuatazo:

1. Kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi,
2. Kuongezeka mapato yatakayolipwa Serikalini kupitia gawio na kodi za mashirika hayo,
3. Kuweza kuzisimamia Taasisi zote zinazojitegemea zikiwemo Kampuni, Mashirika na Taasisi zenye kujiendesha kibiashara.
4. Kuwa na mipango ya kibiashara na mikakati kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa,
5. Kuingia Mikataba baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Bodi ya Wakurugenzi kutapelekea kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao,
6. Kuwepo na udhibiti wa usimamizi wa matumizi ya Mali za Umma,
7. Ofisi ya Msajili ya Hazina itaweza kuzishauri Serikali katika masuala ya uwekezaji wa mitaji ya Umma.

8. Kuimarisha maadili ya utawala bora katika Taasisi za Uwekezaji za Umma.

6. Maelezo ya Mswada wa Sheria

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa marekebisho yaliyofanywa kwa asilimia kubwa, hivyo inalazimika kuifuta sheria ya Mitaji ya Umma nambari 2 ya mwaka 2002 na kutungwa sheria mpya. Mswada wa sheria mpya una jumla ya vifungu themanini na moja (81) ukilinganisha na vifungu thelathini na tano (35) vya sheria ya awali.

Mheshimiwa Spika, Mswada huo umegawanyika katika Sehemu Kuu Kumi kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza: inaelezea masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina fupi na kuanza kutumika,

matumizi na ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika katika Mswada huu.

Sehemu ya Pili: inapendekeza masharti yanayohusiana na kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Sehemu hii inajumuisha masharti ya kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, muhuri na nembo ya Ofisi, kazi na uwezo wa Ofisi. Sehemu hii pia inaelezea kuhusiana na uteuzi wa Msajili wa Hazina, kazi za Msajili wa Hazina, uwezo wa kukasimu majukumu, watendaji wa Ofisi na katazo kwa Msajili wa Hazina na Watendaji.

Sehemu ya Tatu: inaweka masharti yanayohusika na kuanzisha kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma. Sehemu hii inaelezea kwa kina juu ya masharti yanayohusiana na utaratibu wa kuanzisha Taasisi za Uwekezaji za Umma, uwasilishaji wa mapendekezo ya

mradi, hadhi ya kisheria ya Taasisi za Uwekezaji za Umma.

Sehemu hii pia inahusika na masharti ya uteuzi wa Afisa Mtendaji Mkuu, ajira za watendaji, masharti ya utumishi kwa watendaji, muundo wa Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, Bodi ya Wakurugenzi, katibu wa Bodi, muda wa Bodi, ukomo wa kuwa mjumbe, kuvunjwa kwa Bodi, majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi, Kamati za Bodi, Mikutano ya Bodi, kueleza maslahi ya mjumbe, maslahi ya Bodi na Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Sehemu ya Nne: inaweka masharti ya Uwajibikaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma. Sehemu hii inaelezea juu ya mpango mkakati, mkataba wa utendaji wa Afisa Mtendaji Mkuu, tathmini ya mkataba wa utendaji na mikataba ya Utendaji kwa wajumbe wa Bodi. Sehemu

hii pia inaelezea kuhusu masharti ya utayarishaji wa mpango wa fedha, uwezo wa kukopa, uwezo wa kuwekeza, utayarishaji wa taarifa za fedha, matawi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, kuwasilisha malipo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, na fedha na rasilimali za Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Sehemu ya Tano: inahusika na masharti ya kuwasilisha taarifa katika Ofisi. Sehemu hii inajumuisha masharti yanayohusika na wajibu wa kuwasilisha taarifa na utaratibu kwa kuwasilisha taarifa.

Sehemu ya Sita: imeeleza kwa kina masharti kuhusu ukaguzi na uchunguzi ambayo yanajumuisha uteuzi wa wakaguzi, uwezo wa kukagua, uwezo wa mchunguzi na taarifa ya uchunguzi.

Sehemu ya Saba: inapendekeza masharti yanayohusiana na kuunda upya kwa Taasisi za Uwekezaji za Umma.Sehemu hii inaeleza masharti ya pendekezo la kuunda upya, hatua za dharura juu ya usimamizi wa mpito juu ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma, tangazo la kuvunja, uteuzi wa mfilisi na kuvunja Taasisi ya Uwekezaji ya Umma.

Sehemu ya Nane: imeelezea masharti kuhusu Usimamizi wa mali za umma na inatoa majukumu ya Afisa Masuuli, kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali. Sehemu hii pia inaelezea masharti kuhusu Mfumo wa Usimamizi wa Mali, matumizi ya mali za umma, kupatikana kwa mali za umma, umiliki, usajili na uwekaji wa alama, uchakavu na uthamini. Sehemu hii pia inaelezea masharti ambayo yanajumuisha masharti ya kutaifisha mali, uhaulishaji wa mali za umma, ukarabati na uondoaji wa mali za umma.

Sehemu ya Tisa: inaweka masharti ya Fedha ambayo yanajumuisha fedha za Ofisi, bajeti, hesabu na ukaguzi, na Taarifa ya Mwaka.

Sehemu ya Kumi: inaelezea Masharti Mengineyo ambayo yanajumuisha majukumu ya Waziri, masharti ya mpito, kanuni, kufuta na kubakiza Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.